ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Tisa - Tarehe 28 Juni, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe.Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 51

Muelekeo wa Serikali kupambana na Ufisadi na Kutowajibika

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Moh'd Shein wakati akizindua Baraza la Wawakilishi alitangaza muelekeo wa Serikali yake kuwa atapambana na vitendo vya rushwa, ufisadi, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kukosekana kwa uwajibikaji kwa madhumuni ya kuimarisha misingi ya Utawala Bora kwa kutumia Sheria ya Rushwa na ile ya Maadili ya Viongozi.

a) Ni Watendaji Wakuu na Viongozi wangapi mpaka sasa wamechukuliwa hatua kwa makosa ya kutumia vibaya madaraka, na kujihusisha na vitendo vya ufisadi na kushindwa kusimamia uwajibikaji.

b) Kwa kuwa lengo la Mhe. Rais, kuona Serikali yake inatekeleza kasi ya mabadiliko kwa kusimamia misingi ya Utawala Bora, ni hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa za kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima zikiwemo safari za nje, semina na makongamano kama alivyo ahidi katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza.

c) Kwa kuwa wananchi katika kipindi cha muda mfupi wameonesha kufarijika sana na kasi inayoendelea kuchukuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli ya kupambana na tatizo la ufisadi na uwajibikaji, Zanzibar tumejifundisha nini kutokana na mafanikio yanayoendelea kupatikana katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 51 lenye vipengele (a), (b) na (c) lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekua ikichukua hatua mbali mbali katika kupambana na vitendo vya Rushwa, Ufisadi na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa lengo la kuimarisha Utawala Bora. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia rushwa na Uhujumu wa Uchumi, pia, kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi. Miongoni mwa majukumu ya vyombo hivi ni kufanya uchunguzi wa malalamiko yanayohusu tuhuma za vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi pamoja na kuimarisha maadili ya viongozi mkiwemo nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa jumla ya watendaji (10) wamelalamikiwa kwa tuhuma za matumizi mabaya ya Ofisi na watendaji wengine (12) wamelalamikiwa kwa tuhuma za rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, tayari kesi (1) inaendelea na hatua za Mahakama na majadala yasiopungua (4) ya aina hiyo uchunguzi wake umekamilika na tayari yameshawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*).Malalamiko mengine yanaendelea kuchunguzwa katika hatua mbali mbali za uchunguzi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima ya fedha za umma ikiwemo:-

i. Kuzuwia matumizi ya fedha za Serikali kwa kugharamia safari za nje zisizokua za lazima kwa watumishi wa umma na viongozi mkiwemo nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi;

Mhe. Mwenyekiti, naomba kurejea hili la mwanzo ili kutoa msisitizo zaidi kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Kuzuia matumizi ya fedha za serikali kwa kugharamia safari za nje sizizokuwa za lazima kwa watumishi wa umma na viongozi mkiwemo nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi.

ii. Kupiga marufuku matumizi ya fedha za Serikali kwa kuwalipia watumishi wa umma wanaoshiriki katika semina, mikutano, warsha na kongamano.

iii. Kupiga marufuku malipo ya watumishi wa umma kwa kazi inayofanywa ndani ya saa za kazi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mafunzo yanayopatikana kutokana na hatua zinazochukuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika kupambana na tatizo la rushwa, uhujumu wa uchumi na uwajibikaji ni pamoja na haya yafuatayo:-

i. Vita dhidi ya rushwa na ufisadi vinahitaji mashirikiano ya pamoja kati ya viongozi wangazi zote na wananchi kwa ujumla;

ii. Umuhimu wa viongozi kufuatilia majukumu yao na kusimamia maagizo yanayotolewa na Serikali kwa nia ya kusimamia utekelezaji wake;

iii. Umuhimu wa sisi viongozi kutekeleza kwa vitendo ahadi tulizozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni na;

iv. Umuhimu wa kujali maslahi ya umma na kuwa wazalendo kwa nchi yetu. Ahsante Mhe. Mwenyeki.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa nini idadi ya ma-*files* yenye kuchunguza ni mengi kuliko kesi zilizofikishwa Mahakamani wakati vitendo vinavyofanyika vinarudisha nyuma na maendeleo ya Zanzibar kwa wananchi wake.

(a) Je, serikali inatoa kauli gani.

(b) Kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo imeshajengewa ghofu na kuwepo ufisadi na ushahidi ndani ya Baraza hili ikiwemo *Airport*, *AGAPE* na Skuli za Sekondari. Mamlaka hii imeanza lini kuchunguza hali ya kuhujumu uchumi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Mhe.

Jaku Hashim Ayoub, arejee maswali yake kwa sababu sijayafahamu vizuri na ende taratibu ili niweze kufahamu vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa nini idadi ya ma-*files* yenye kuchunguzwa ni mengi kuliko kesi zinazofikishwa Mahakamni wakati vitendo vinafanyika vinarudisha nyuma maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake.

(a) Serikali inatoa kauli gani kuhusu kadhia hiyo? Nafikiri umenifahamu Mheshimwa.

(b) Kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo imeshajengewa ghofu na wananchi kwa kuwepo ufisadi na ushahidi ndani ya Baraza hili jana limezungumzwa suala hili, nyuma limezungumzwa suala hili kwa mfano; *Airport*, *AGAPE* na Skuli za Sekondari, taasisi yako imechukuwa hatua gani ya kuchunguza rushwa katika vitengo hivi nilivyovitaja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wawakilishi, waelewe kwamba wanapotathmini taasisi au Mamlaka ya Rushwa wasiangalie moja kwa moja tathmini ile kuangalia kesi ngapi ambazo zimepelekwa Mahakamani au madai mangapi ambayo yamepelekewa Mahamakani. Kuna mambo mbali mbali ambayo Mamlaka hii ya Rushwa unafanya katika kazi zake za kila siku, kwa mfano katika kipindi hiki cha karibuni katika taasisi hii imepambana na rushwa na uhujumu uchumi imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba mapato ya serikali hayapotei.

Taasisi hii ilishughulikia kikamilifu wale wakwepa kodi ambao wanajaribu kukimbia kimbia wanaohusiana na Shirika la nyumba. Katika Shirika la Nyumba Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna walipaji ambao kwa njia moja au nyengine wanajaribu kukwepa kodi. Sasa ni taasisi hii ambayo iliopelekea kuhakikisha kwamba zile fedha ambazo wanaotakiwa wale walipa kodi katika Shirika la Nyumba zinalipwa na tunashukuru kwamba fedha nyingi Shirika hili la nyumba imezipata kutokana na jitihada hii ya taasisi au Mamlaka hii ya Rushwa.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, wasiangalie hii taasisi kuitathmini na kuangalia utendaji wao kwa kuangalia kesi ngapi ambazo zimepelekwa Mahakamani. Kuna mambo mengine ambayo vile vile yanafanywa na taasisi hii na sio kwamba unapomkamata mtu moja kwa moja tu umpeleke Mahakamani. Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mbali mbali ambayo

yanatakiwa kufanywa ile kesi yako iweze kupelekwa Mahakamani. Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii iko mstari wa mbele kuhakikisha kwamba yale makontena ambayo yanashushuwa pale Bandarini yanakaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ulivyo ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara huwa wanaleta makontena yao lakini kile ambacho walichoki-*declare* sicho ambacho kilichokuwemo kwenye makontena. Sasa taasisi hii pamoja na mambo mengine inashughulikia kuhakikisha kwamba kile kilicholetwa au kilichotangazwa na wale wafanyabiashara kwenye zile kontena ndicho ambacho halisi kilichokuwepo na kama sicho wanatakakiwa vile vile kwa utaratibu ambao upo pale wanatoza faini ili kuhakikisha kwamba kodi ya serikali inaingia.

Kwa hivyo, madai ni mengi kuliko kesi, sasa kama nilivyokwambia awali kwamba kupelekwa kesi Mahakamani kunahitaji matayarisho mbali mbali ili kesi ile iweze kupelekwa Mahakamani, kwa sababu tunapopeleka Mahakamani kesi ambayo haina matayarisho ni sawa sawa kuipa kazi Mahakama kule nyingi zitakuwepo kesi ambazo hatimae zitakuwa hazina mwisho mwema kwa sababu hazina ushahidi wa kutosha.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu, kifungu cha 37, nafikiri Mhe. Naibu Waziri, hakunisikia, bora nirudie tena maswala, maana yake nimeuliza njia ya kwendea *Airport,* ananambia nipite Bububu, siwezi kufika *Airport,* naona nirudie tena. Nilichouliza sicho nilichojibiwa. Naomba usikilize kidogo Mhe. Naibu Waziri kwa makini.

(a) Kwa nini idadi ya ma-*files* yenye kuchunguzwa ni mengi kuliko kesi zinazofikishwa Mahakamni. Kwa ufupi tu, nimefupisha.

(b) Kwa kuwa miradi mingi ya maendeleo imeshajengewa khofu na wananchi, kupitia mamlaka yako taasisi ngapi imeshachunguza. Ndio nilioiuliza mimi, madogo tu hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Narejea kusema kwamba ili kesi iende Mahakamani kuna mambo mengi ambayo yanatakiwa kufanywa ile kesi ile iende Mahakamani pamoja na kukamilika kwa ushahidi. Kwa hivyo, kwa ufupi nikujibu kwamba;

(a) Kesi zinachelewa kufika Mahakamani kwa sababu ushahidi unakuwa mdogo.

(b) Taasisi yangu au Mamlaka yangu ya kuzuia rushwa iko mstari wa mbele kushirikiana na taasisi mbali mbali zikiwemo za serikali kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanashutumiwa katika suala zima la rushwa wanachukuliwa hatua. Sasa pamoja na mambo mengine hili mara tu litakapofika ofisi kwetu mambo yote ambayo umeyaeleza tutayasimamia na kuyachukulia hatua ili kuhakikisha kwamba wale wote wabadhirifu waliofanya mambo haya wanachukuliwa hatua ipasavyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa azma yake nzuri ya kuhakikisha kwamba tunajitoa katika maficho na tunaingia katika utandawazi ili kuleta maendeleo ya haraka na kuwatumikia wananchi wetu ipasavyo.

Lakini kwa bahati nzuri baada ya kauli yake hiyo wasimamizi wakuu ni Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wengine.

(a) Je, mpaka sasa hivi kufikia hatua yetu tuliokuwa nayo karibu ya miezi mitatu sasa hivi, tumefikia hatua gani nzuri ya kuridhisha juu ya utendaji wetu katika taasisi zetu.

(b) Kuna baadhi ya watendaji katika serikali yetu hii tuliokuwa nayo baadhi ya taasisi hawakamilishi utendaji wao mzuri, mara nyingi huchukuwa mazungumzo mengi kuliko utekelezaji, hawa wanachukuliwa hatua gani ili kuhakikisha kwamba serikali yetu inaendeleza juhudi ya kuwakwamua wananchi wetu ili wawe katika maisha bora na utawala bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Zanzibar itahakikisha au inahakikisha kwamba mambo yote yanahusiana na utekelezaji wa Watumishi wa Umma au masuala yote yale ambayo yanayotakiwa kutekelezwa na Utumishi wa Umma masuala haya yanafanywa na tutahakikisha kwamba tutafatilia kwa ukaribu kuhakikisha kwamba utendaji bora wa wafanyakazi wetu unakuwa na ufanisi zaidi.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake Mhe. Waziri, alisema idara ya kuzuia rushwa na kuhujumu uchumi imekuwa ikiwatafuta wasiolipa kodi, sasa mimi suala langu liko hapa.

Wasiolipa kodi ni wala rushwa, mbona hii taasisi sasa inaanza kutoka katika mstari wakati ina jukumu la kuwatafuta wala rushwa na wahujumu uchumi. Kuna watu wanakaa katika nyumba za serikali kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri, ambao idara hii inawatafuta na kuwataka ku-*harass* ili wakalipe kodi. Sasa huoni kama hapo inafanya jukumu si lake. Mtu anakaa nyumba ya serikali, idara ipo ambayo ina jukumu la kuwakumbusha kulipa kodi. Lakini sasa idara nyengine ndio inafanya kazi ambayo mimi nahisi sio yake.

Naomba mlipa kodi mwenye kukaa nyumba ya serikali inahusika nini na Idara ya Rushwa na kuhujumu Uchumi kwenda kushughulikia kazi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba ieleweka kwamba Taasisi hii ya kuzuia Rushwa sio kwamba kazi yake tu iliyopewa na sheria kuzuia rushwa. Lakini pamoja na mambo mengine yakiwemo hayo masuala ya ufatiliaji wa hao walipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile nimueleze Mhe. Hassan, kwamba Taasisi yangu ilipokuwa ikifanya huo utaratibu wa kuwafuatia hawa ambao walipa kodi walikuwa hawa-*harass* au hawawafanyii vitendo vya nguvu ili kuweza kulipa kodi, sijasema hilo. Nilichosema ni kwamba taasisi yangu pamoja na mambo mengine imeandaa mbinu mbali mbali ambazo zinatumika ili hawa walipa kodi wamepelekea kuweza kulipa kodi vyengine, siyo taasisi yangu kwamba inatumia njia za nguvu, njia za *harassment* kuhakikisha kwamba hawa watu wanabanwa kulipa kodi, hapana. Isipokuwa ina mbinu zake za kitaalamu ambazo Mheshimiwa, sasa mimi na wewe inawezekana tusizijue, lakini wao ni wataalamu wanajua namna gani ku-*deal* na wananchi kwa *level* tofauti.

Nam. 16

Kusaidiwa kwa Vijana ambao Wazee wao Hawana Uwezo

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliondosha swali langu Nam. 16 kwa sababu majibu tayari yameshatolewa katika hotuba ya Mhe. Waziri. (*Makofi*)

(Swali hili limeondoshwa na Mhe. Mjumbe aliyetaka kuliuliza)

Nam. 94

Ukosefu wa Huduma ya Maji ya Uhakika

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kny: Mhe. Shehe Hamad Mattar) – Aliuliza:-

Naomba ninukuu maneno ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Hotuba yake wakati wa uzinduzi wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar, "Alisisitiza kwamba ushirikiano katika kuimarisha huduma za jamii, ambayo pamoja na huduma ya maji. Na kwa kuwa katika Jimbo la Mgogoni lililopo Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna Shehia kama vile Shehia ya Finya, Taifu, Kinyasini, Mgogoni ambazo kwa muda mrefu sana hazipatiwi huduma ya maji kwa uhakika jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa sana kwa waakazi wa maeneo hayo na kuikosesha Serikali mapato kupitia huduma hizo. Na kwa kuwa katika Jimbo la Mgogoni kumejengwa tangi kubwa sana kwa ajili ya kuhifadhia maji katika kijiji cha Taifu na pia kuchimbwa visima (vingi) katika Shehia ya Mgogoni kikiwemo kisima kimoja kilichochimbwa hivi karibuni katika eneo la kambi ya FFU Finya.

a) Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa maeneo hayo huduma hiyo ya maji kwa uhakika ili kuondokana na usumbufu wanaoupata hasa akina mama na kuongeza mapato katika nchi.

b) Je, kisima hicho kilichochimbwa eneo la Finya katika eneo la kambi ya FFU kitaanza lini kutumika ili wananchi wafaidike na huduma hiyo ya maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 94 kama ifuatavyo:-

Ni kweli wananchi wa Shehia za Finya, Taifu, Kinyasini, Mgogoni wamekuwa na tatizo la uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji ya uhakika kwa kipindi kirefu. Ni sahihi pia kwamba kuna tangi kubwa la kuhifadhia maji eneo la Taifu pamoja na visima vitano katika bonde lililopo katika Shehia hiyo. Hata hivyo, tangi hilo na visima hivyo vinahudumia Mji wa Wete.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imeshachimba visima vitatu katika maeneo ya Kifundi, Kwalegongo na Finya FFU. Hatua zinazofuata ni kuvipima visima hivyo *(pumping test)* kujua uwezo wake wa kuzalisha maji pamoja na kuviendeleza kwa kujenga vituo vya maji sambamba na kuvuta umeme na kuviunganisha na mitandao ya bomba za maji iliyopo katika maeneo hayo. Kwa hatua za awali, Kituo cha Kisima cha Finya FFU kimeshaanza kujengwa na kitafuatiwa na kile cha Kifundi kutokana na gharama ndogo za umeme zinazohitajika kukamilisha ujenzi huo.

Ahsante, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yako mazuri lakini naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Je, ni lini kisima hicho kilichochimbwa eneo la Finya FFU ni lini kitaanza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kisima hicho kitaanza kazi punde baada ya kukamilika kwake lakini ndani ya bajeti ya 2016/2017.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Katika Jimbo langu la Tumbe Shehia ya Shumba Viamboni wizara ilichimba kisima na wanatakiwa wananchi pale wajenge kibanda kwa ajili ya matumizi mazima ya kile kisima. Lakini tokea mwaka 2014, hadi leo kisima kile hakijatumika na wale wananchi huduma hawajaipata. Ni lini sasa kisima kile kitafanya kazi na wananchi waanze kupata maji kama kawaida.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Baada ya kuipata hiyo taarifa tutawasiliana na wataalamu wetu wa *ZAWA* kwa ajili ya kuona tatizo ni nini na kwa kushirikiana naye ninamuahidi kwamba tutalifanyia kazi, *in shaa Allah.*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba kumuuliza swali la ziada Mhe. Naibu Waziri, lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa serikali inajitahidi sana kuchimba visima kusaidia wananchi kupata maji masafi na kwa wingi.Visima vingapi serikali imeshachimba na vingapi vinatoa huduma na vingapi vimefeli ambavyo havitoi huduma.

(b) Ni sababu zipi ambazo zimesababisha hasara ya hivi visima ambavyo vilivyochimbwa vikafeli wakati kunatakiwa mwanzo wafanye uchunguzi ili wahakikishe kwamba maji yanapatikana safi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kwa vile swali la (a) ni la takwimu basi nitamuomba nimjibu kwa maandishi kwamba visima vingapi vimechimbwa na vingapi vinafanya kazi na vingapi havifanyi kazi.

(b) Ni kwamba kabla ya kuchimbwa visima utafiti wa kina unafanywa. Niliwahi kusema siku moja hapa kwamba baadae yanatokezea mambo mengine ya *natural hazard* ambayo yapo nje ya uwezo.

Lakini ni kwamba swali la (a) kama nilivyokuwa nimesema basi nitamjibu kwa maandishi, ninadhani nimemjibu.

Nam. 206

Upatikanaji wa Huduma ya Umeme

Mhe. Said Omar Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa utaratibu wa kufikisha umeme katika kila Shehia Unguja na Pemba, Mijini na Vijijini.

(a) Je, Wizara na Shirika linayo habari kwamba umeme haujafikishwa katika vijiji vya Mafya na Kitaalani katika Shehia ya Wingwi na Rahaleo, Mnazimmoja na Kibondeni katika Shehia ya Sizini.

(b) Lini *ZECO* kwa kushirikiana na Wizara itafikisha umeme katika vijiji hivyo.

(c) Huoni kuendelea kuchelewa kufikisha umeme katika vijiji hivyo ni kuwanyima wananchi maendeleo ya vijiji hivyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 206 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kitakwimu ni Shehia mbili tu kwa Unguja na Pemba ambazo bado hazijapata huduma ya umeme ambazo ni Minazini na Kisiwa cha Fundo. Lakini kwa upande wa vijiji, mpaka sasa Serikali imefanikiwa kusambaza umeme vijijini kwa asilimia 86. Hivyo, azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba asilimia iliyobaki ya vijiji ambavyo havijapata umeme vitakamilishwa kusambaziwa umeme katika kipindi cha miaka minne ijayo hatua kwa hatua. Zoezi hili linamaanisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuwa ifikapo mwaka 2020 vijiji vyote vilivyosalia viwe vimeshapata huduma ya umeme.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuwa azma ya serikali ni kuwapunguzia wananchi wake ukali wa maisha na kuwapa msukumo wa kidharura kwa yale mazito yaliyokuwa hawayamudu kama hili la umeme. Je,wizara yako itaisaidiaje serikali kufikia azma yake hiyo ili wananchi wa vijiji vya Wingwi na Sizini wapate huduma hiyo ya umeme.

(b) Kwa kuwa Baraza lipo ukingoni kumalizika tena. Lini utatembelea vijiji hivyo ili uvione kwa macho kabla ya kufika huduma hizo ili hawa wananchi wajenge imani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, lile la kwanza nimemsikiliza kwa makini lakini sijamuelewa, naomba arejee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Said Omar Said, naomba urejee swali lako ili alielewe Mhe. Naibu Waziri, aweze kujibu.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Mwenyekiti, swali langu la mwanzo ninasema, kwa kuwa azma ya serikali ya kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi na kuwapa msukumo wa kidharura kwa yale mambo mazito waliyokuwa hawayamudu kama hili la umeme. Je, wizara yako itaisaidiaje serikali kufikia azma yake hiyo ili wananchi wa vijiji hivyo wafaidike na huduma ya umeme.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Ni kweli kwamba azma ya serikali ni kuhakikisha kwamba kwenye vijiji vyote tunapeleka umeme na kama alisikiliza kwa makini katika jibu la msingi tulisema kuwa mpaka kufikia mwaka 2020 vijiji vyote tuna azma ya kwamba tayari viwe vimeshapata huduma ya umeme, lakini tunakwenda kwa awamu.

(b) Kuhusu lini tutatembelea. Ni baada ya kumaliza shughuli za Baraza tutakuwa na nafasi nzuri ya kutembelea katika Shehia zote kuhakikisha kipi kinahitajika kifanyike.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali la ziada lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa wizara nyingi kama hii yao duniani hupelekea watu nguzo za umeme pamoja na umeme mpaka karibu na maeneo yao na kuwa-*charge* ile *amount* ambayo ya kuingiza ndani ya nyumba huo umeme. Ni sababu zipi zinazowafanya wizara hii kuwa-*charge* hawa wananchi wanapotaka umeme nguzo pamoja na waya za umeme baadhi ya wakati pamoja na kutia umeme ndani ya nyumba yao wanawa-*charge* vile vile.

(b) Je, wizara hii haioni kwamba inawaangusha kimapato zaidi kiuchumi wananchi hawa waliokuwa hali ya chini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Alisema kwamba ni mambo gani yanayopelekea serikali i-*charge* wananchi. Ni kwamba azma ya serikali kuhakikisha tunapeleka umeme vijijini mote lakini kwa awamu ama mpango ambao shirika unao. Na tunapeleka kama nilivyosema kwa awamu, kinapotokezea kijiji kinaharakisha kutaka ule umeme yanatokezea hayo ambayo unayasema. Kwa hivyo, ni lazima wachangie, lakini la pili inategemea mfuko uliokuwa upo kwenye serikali kwa wakati huo. Lakini licha ya hayo yote ni kwamba shirika linafanya jitihada ya kuhakikisha umeme unafika kwa bei nafuu.

Kwa sababu kama utaangalia nguzo tunachukua kwa takriban laki nne kutoka Afrika Kusini, lakini tunakuuzia ama tunakuchangisha kwa laki moja na thamanini. Sasa si kwamba unauziwa bali ni ile jitihada ya serikali kuhakikisha kwamba unapata huduma hii katika kijiji.

(b) Hatuoni kwamba tunawakwamisha wananchi kiuchumi, labda ueleze wewe kwa nini. Lakini sisi hatuoani hivyo, kwa sababu huwa tunawasaidia wananchi wetu kwa bei nafuu na hata kama tulivyokuwa tumesema huko nyuma tunachukua umeme kwa mia mbili na sabini na tano, lakini wewe tunakuuzia kwa shilingi mia mbili na ishirini na mbili, hatuoni sababu ya kwamba tunawakwamisha wananchi kiuchumi.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza tena swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri, Shirika la Umeme linawapelekea wananchi huduma hii kwa ukaribu ili kuondoa usumbufu wa huduma wanayohitaji. Sasa kule Pemba shirika limeweka vituo vyake sehemu mbili. Moja ni Chake Chake na pili ni Wete.

Sasa je ni mpango gani wa Wilaya yetu ya Micheweni mutaufanyia ili kuweka kituo hichi karibu ukiangalia kwamba wananchi tunaoishi ndani ya Wilaya ile tunapata usumbufu, watu waondoke waende Chake Chake na Wete hasa ukilinganisha katika kipindi hichi zaidi kuna siasa mbaya hata mtu ukamtuma kama ana gari yake nichukulie umeme, basi hakuletei.

Ni lini sasa mutaweka kituo hichi pale karibu Wilaya ya Micheweni pamoja na mafundi ambao kukitokezea hitilafu tukaweza kupata huduma hii.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Lakini la pili tunategemea turudishe ile huduma ya kununua umeme kwenye simu kwa kuepusha hayo haraka iwezekanavyo.

Nam. 31

Utaratibu wa Kusafirisha Wagonjwa Nje ya Nchi

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Wizara ya Afya imekuwa ikitumia Bilioni 2 kusafirisha wagonjwa nje ya nchi kwa mwaka, kwa mujibu wa Bajeti ya mwaka 2015/2016. Kwa kuwa utaratibu wa kununua vifaa na kuleta madaktari bingwa kuja kutoa huduma hizo Zanzibar kwa wagonjwa wanaotakiwa kutibiwa nje ya nchi ili wananchi wengi wanufaike badala ya kusafirishwa ni utaratibu mzuri zaidi ambao utasaidia kupunguza malalamiko kwa wananchi.

a) Tanzania Bara imeshaanzisha mpango huo kwa madhumuni ya kunufaisha wananchi walio wengi, je, lini Serikali yetu itaanza utaratibu huo.

b) Je, Serikali haioni kuwa utaratibu wa kuleta madaktari ndio njia pekee ya kuondoa malalamiko hayo.

c) Ni mahitaji gani yanakosekana katika hospitali yetu tegemeo ya Mnazi Mmoja hadi wagonjwa wapelekwe nje ya nchi kwa matibabu wakati tunaambiwa madaktari bingwa wapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

(a) na (b), Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kuchukua Madaktari kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kutoa huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja ulianzishwa tokea mwaka 2008, ambapo kwa kuanzia huduma za *plastic surgery* na ngozi zimekuwa zikitolewa kwa wananchi wote wa Zanzibar na baadae zikafuatiwa na huduma za matatizo ya Ubongo na Uti wa Mgongo *(Neuro surgery)* ambazo zilikuwa zinatolewa na madaktari kutoka Spain.

Aidha, ili kuondoa malalamiko kwa wananchi, Wizara imeshajenga jengo la huduma za matatizo ya Ubongo na Uti wa Mgongo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na huduma katika jengo hilo tayari zinaendelea kutolewa. Hospitali ya Mnazi Mmoja kila mwezi huendesha kambi maalum zinazojumuisha madaktari wetu na wageni ambao ni bingwa wazalendo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma za hali ya juu na kwa unafuu. Madaktari hawa wanatokea nchini Spain kwa mkataba kupitia Shirika la *NIL*.

(c) Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuwepo kwa madaktari bingwa ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambao hushirikiana na madaktari wetu wazalendo, bado Hospitali yetu haijajitosheleza kwa baadhi ya huduma hususan kwa matatizo makubwa ya moyo na saratani ambapo hata wenzetu wa Tanzania Bara hupeleka baadhi ya wagonjwa wenye matatizo makubwa nje ya nchi kwa matibabu. Hata hivyo, ni wagonjwa wachache ukilinganisha na orodha yote ya wagonjwa ambao hospitali yetu ya Mnazi Mmoja hulazimika kuwasafirisha nje ya nchi ili kupata matibabu hayo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaamini kwamba ili kupata matibabu mazuri na kutegemea wataalamu kutoka nje ni sehemu moja ya kuongeza wataalamu wetu kupata ujuzi zaidi. Swali langu lipo hapa.

(a) Je, Wizara ya Afya kupitia Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ina madaktari bingwa wangapi.

(b) Madaktari hao ni wa fani gani.

(c) Kuna kitu gani kinachosababisha vitendea kazi baadhi vingi vinakosekana kwa utaratibu wa kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, utajibu maswali mawili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba radhi kuhusu madaktari bingwa wangapi, hili nitakujibu kwa maandishi kutokana na kuwa sina takwimu sahihi ni wangapi.

(b) Hospitali ya Mnazi Mmoja ina mpango gani wa kupata madaktari zaidi, hasa baada ya bajeti yetu kupita, kwa sababu tutakuwa na uajiri na tanawatangazia rasmi wale ambao wanafanya udaktari, tunawahitaji katika Serikali yetu hii ya Zanzibar, ili watoe huduma kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo, baada ya bajeti yetu kupita vizuri na tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe muipitishe vizuri, ili malengo haya yafanikiwe na tuweze kupata madaktari wenye hadhi ili kuwatibu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, na kwa bahati nzuri baada ya kipindi cha maswali na majibu, tutakuwa na mswada ule wa Mnazi Mmoja pia watapata kujua mambo mengi Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) aliuliza kuhusu takwimu. Swali la pili ambalo Mhe. Naibu Waziri kalijibu vizuri sana, naomba kuongeza majibu hapa.

Hivi sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja ina jumla ya wafanyakazi 1,181, kati ya hao madaktari bingwa ni 21 na madaktari wale *General Practitioners* yaani madaktari *MD, Medical Degree* ya Kwanza kabisa ni 103. Kwa hivyo, jumla ya madaktari wote ni 124 wa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili alilouliza Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), namshukuru sana kwa swali lake zuri, kwa sababu huku tunakoelekea sasa hivi Hospitali ya Abdalla Mzee tunatarajia itafunguliwa mwezi wa Septemba, patahitajika madaktari na wafanyakazi wengi sana. Baada ya hapo kuna ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, alipokuwa akiwaomba ridhaa wananchi aliitoa juu ya Binguni, nako kutahitajika madaktari wengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti *speech* yetu tulieleza kwamba haijapata kutokezea mwaka, katika historia ya Zanzibar, ambapo tumekuwa tukiwasomesha madaktari wengi sana, kama mwaka huu, wote jumla ni 137 ambao wako masomoni, pamoja na kada nyengine mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu, tumeanzisha *degree programme* yetu wenyewe sasa hivi, ambapo *bench* ya mwanzo kabisa wale waliosoma chini ya Cuba, *Matanzas University* walikuwa vijana 38. Ni mara ya kwanza katika historia ya Zanzibar kutoa madaktari wake wenyewe, ambao ni wazalendo na wamesoma hapa hapa.

Hivi sasa tuna vijana takriban kama 90 hivi ambao wanasoma *SUZA* na wao wakimaliza pia wataongezea ile *pool* ya madaktari, mambo yatakapofunguliwa kule Hospitali ya Abdalla Mzee na baadae *In shaa Allah* Binguni. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Tatu Mohamed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo tu la nyongeza. Je, ni wagonjwa wangapi tunaowasafirisha nje ya nchi kupata matibabu kwa kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwa mwaka 2015/2016 wizara imesafirisha wagonjwa 342, wakiwemo wagonjwa wa maradhi tofauti; saratani, moyo, mafigo na matatizo mengine kwa watoto na watu wazima.

Nam. 104

Uharibifu wa Shamba la Miwa Mahonda

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha hivi karibuni tumeshuhudia hujma ya uchomaji moto mashamba ya miwa yanayomilikiwa na Kiwanda cha Sukari Mahonda na kupelekea hasara kubwa.

a) Je, ni hasara gani kiwanda hicho imepata kutokana na hujma hiyo ya moto.

b) Je, ni watu wangapi wamekamatwa katika kadhia hiyo.

c) Je, Serikali imejipanga vipi kuona hujma kama hii haitokei tena.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na hujuma za kuchoma moto miwa katika mashamba ya Kiwanda cha Sukari Mahonda.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichoanzia mwezi wa Disemba 2015 mpaka Aprili 2016, jumla ya matokeo manane ya hujuma za uchomaji moto zilifanyika, ambapo ekari 834 za miwa zimechomwa moto. Hasara iliyopatikana kutokana na uchomaji huo inakadiriwa kufikia Dola za Kimarekani milioni 4.7.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kuhusiana na hujuma hizo, lakini matukio yote ya hujuma yaliripotiwa katika Kituo cha Polisi Mahonda, ambapo uchunguzi unaendelea.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ili kukabiliana na hujuma hizo, serikali inaendelea na mazungumzo na Uongozi wa Kiwanda, kuona jinsi ya kuimarisha ulinzi wa mashamba ya miwa na kiwanda kwa ujumla.

Vile vile, serikali inaendelea kuwanasihi wananchi wa Zanzibar, na hasa wale wanaopakana na mashamba ya mradi huo, kuwa wavumilivu. Wasivunje Sheria kwa kufanya hujuma za aina yoyote kwa mali za miradi ya wawekezaji. Kwani kufanya hivyo ni kinyume na sheria za nchi, na vile vile inaikosesha serikali mapato ambayo yanasaidia sana katika kuendeleza huduma za kijamii katika nchi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, naomba nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwa kuwa katika majibu yake mama alikiri kwamba hadi sasa hivi hakuna mtu yeyote aliyekamatwa.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea watu hao kutokukamatwa hadi leo.

(b) Tunajua kwamba Kiwanda cha Sukari cha Mahonda kimeanzisha bidhaa yake ya sukari ya kisiwa, ni lini itaingia sokoni bidhaa hiyo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

(a) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba kesi zao bado hazijafikia mahali pa kupelekwa mahakamani, ni kwa sababu polisi wanaendelea kufanya uchunguzi ili waweze kuwakamata.

(b) Kuhusu bidhaa, hivi sasa Kiwanda cha Sukari Mahonda walikuwa wamezalisha tani 350 za sukari na tumewaruhusu sukari hiyo kuitia katika soko, kwa hivyo, tegemeeni kupata sukari hii katika soko wakati wowote.

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Ahsante Mhe.Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake amesema kwamba kutokana na uchomaji huo hasara iliyopatikana ni takriban dola milioni 4.7.

(a) Je, serikali katika hizi dola milioni 4.7 serikali imepata hasara kiasi gani katika fedha hizi pamoja na kiwanda pia.

(b) Ni hatua gani zilizochukuliwa na serikali ili kuwapa elimu wananchi walio pembezoni mwa kiwanda hiki, ili kutokufanya tena vitendo hivi ambavyo vinaleta hasara kwa serikali na kwa wananchi wenyewe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kiwanda hiki kimepata hasara kubwa sana, shilingi milioni 4.7 sio hasara ndogo, kwa sababu miche ya miwa imeungua. Kwa hivyo, hasara zimechanganyika na kukosa mapato, kukosa kuuza sukari na bidhaa nyengine zinazotokana na sukari. Kwa hivyo, hiyo ni hasara kubwa kwa upande wa vitega uchumi kwa wazalishaji hawa wa Mahonda.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kubwa serikali imepata hasara, kwamba mapato ambayo yalitakiwa yapatikane kutokana na sukari hii hayatoweza kupatikana, kwa sababu hii sukari ndio imechomwa moto haikuweza kuzalishwa na kuuzwa.

Mhe. Mwenyekiti, swali la pili kama nilivyosema kwenye bajeti yangu tulipokuwa tunajadili bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, nilisema kwamba Wazanzibari wanatakiwa waeleweshwe vizuri sana, umuhimu wa wawekezaji nchini kwetu. Kwa sababu wawekezaji ndio ambao wanazalisha mapato kwa taifa letu, kwa sababu bila ya mapato hata hapa tunazungumzia masuala ya afya na mambo mengine ya jamii yanashindikana, kwa sababu inakuwa hakuna uwezo wa kuendeleza taifa letu kimapato.

Kwa hivyo, inaonekana kwamba bado hii elimu ni ndogo. Nilisema kwamba tutajitahidi kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa na serikali nyengine zilizoko vijijini kwetu. Kwa mfano, Wilaya mpaka kwa Madiwani wetu, ili waeleweshwe na wao wafanye kazi ya kuwaelewesha hasa wananchi.

Tatizo la Mahonda ni kwamba bado kulikuwa kuna ushindani kati ya wananchi ambao wanalima katika maeneo yale na wenye viwanda, wanasahau kwamba kile kiwanda bado ni mali ya Zanzibar, kwa sababu kiko Zanzibar kwa ajili ya kufanya shughuli za Zanzibar na kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kupata kipato. Wao wanapata faida, lakini na serikali pia inapata faida, na sisi wananchi tunapata bidhaa yetu ile sukari iliyokuwa safi kabisa. Tukumbuke sukari iliyokuwa safi ni sukari ya miwa, kuna sukari za aina nyingi. Sukari ya miwa ina bei nzuri, ni safi na inapendwa na watu wengi.

Kwa hivyo, hichi kiwanda ni muhimu kwetu, lakini bado elimu inatakiwa ifike kwa wananchi na tutajitahidi kushirikiana na uongozi wa serikali katika vijiji vya Kaskazini, ili kuwaelewesha umuhimu wa kiwanda hiki, pamoja na mambo mengine ambayo wanayafanya kiwanda hiki kwa ajili ya kuwasaidia wananchi. Ahsante *(Makofi)*

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri. Unajua sasa hivi wafanyabiashara au matajiri wenye magari huwa wanayachukua wakiona yamechoka, wanayapeleka maeneo ya maficho wanayachoma moto ili wapate kulipwa Bima.

Je, na hawa watu wanaozalisha miwa na wao hawaendi kuichoma moto kwa makusudi, ili serikali ipate kuwalipa Bima.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kama nimelifahamu vizuri swali lake, haiwezekani wawekezaji hawa wakachoma miwa kwa makusudi ili walipwe Bima, kwa sababu wakichoma miwa wanapata hasara sio mara mbili au tatu. Kwa sababu wao kazi yao ni kuzalisha miwa kwa ajili ya kutoa sukari. Kwa hivyo, sidhani kama wanaweza kufanya hivyo, na sina taarifa na sitaki kufikiria hivyo, lakini inawezekana wafanyabiashara wengine wanafanya hivyo, lakini sio kwa maslahi ya wenye kiwanda kuchoma miwa kwa makusudi Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Nam. 88

Tatizo la Stendi Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Mji wa Chake Chake kwa muda mrefu sasa umekuwa hauna *stand* ya gari za abiria na mizigo suala ambalo limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwa wananchi na wafanyabiashara wa mji huo. Hata hivyo, serikali mara kadhaa imekuwa ikiahidi kutafuta ufumbuzi wa kadhia hii, lakini mpaka muda huu hakuna mafanikio yoyote.

a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulitatua kwa haraka tatizo hili.

b) Ni lini suala hili litapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutafautiana na Mhe. Mwakilishi kwa kusema kwamba Mji wa Chake Chake hauna *stand*, kwani *stand* ipo, lakini tunaweza kusema haitoshelezi kwa ukweli, lakini serikali inachukua hatua

mbali mbali, ili kuhakikisha inawaondolea shida wananchi wake kwa kuzingatia kuwa maegesho au *stand* iliyokuwepo pale Qatar haitoshelezi.

(a) Mhe. Mwenyekiti, serikali inaona umuhimu wa kulitatua tatizo hili, kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kushirikiana na Baraza la Mji la Chake Chake, la kuwaondoa wafanyabiashara waliokuwa wanafanya biashara katika eneo la *stand* hiyo, na kuwapeleka eneo linaloitwa Qatar, ili kuongeza nafasi ya maegesho kwa gari za abiria, ingawa kama nilivyosema mwanzo pale sehemu hapatoshelezi.

(b)Mhe. Mwenyekiti, siwezi kusema lini itakuwa tayari, kwani maegesho ya *stand* zote ziko chini ya Baraza la Mji la Chake Chake na Halmashauri za Wilaya. Kazi za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni kuzitangaza kwa matumizi baada ya makubaliano ya wizara tatu ambazo zinahusiana na mambo ya ardhi, usafirishaji na Mabaraza ya Mji. Wizara hizo ni Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa bado hakujawa na eneo lililokubalika kujengwa *stand* hiyo, lakini majadiliano na taasisi husika yanaendelea na karibuni tu tutapata maamuzi muafaka na kuyatangaza baadae. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, ndugu yangu rafiki yangu sitaki nipingane naye kwamba Chake Chake hakuna *stand*, lakini majaribio ya karibuni tu gari ziliambiwa ziende *stand* ikawa balaa pale, lakini sitaki niende huko.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niulize swali (a) na (b). Mimi nataka niseme kwamba tukubaliane kwamba Chake Chake tumeifanyia makosa ya kukosa *stand*. Sasa *stand* iliopo pale ambayo Mhe. Naibu Waziri amesema ipo, na *stand* ambayo tunaikadiria kwamba ijengwe na ambayo itakuwa nje ya mji. Kwa muda wa miaka 10 ambayo tunakwenda nayo bado wananchi wetu wa kutoka Konde, Micheweni, Wete, Mkoani na maeneo mengine bado hawajaweza kupanda gari mbili au tatu mpaka wafike mjini.

Kwa hivyo, nilikuwa ninamshauri Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu na mimi ni mdau wa serikali hii. Mimi ningemshauri Mhe. Naibu Waziri kwamba *stand* ambayo ndio anaiita *stand…*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, swali la nyongeza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakuja Mhe. Mwenyekiti, *stand* ambayo inaitwa *stand* ambayo iko Chake Chake iweze kugharamia mji mmoja ama wa Mkoani au wa Wete kwa upande wa Kaskazini. Tukubaliane tu kwamba je…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, uliza swali. Wakati wa kuchangia umeshapita.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Swali linakuja Mhe. Mwenyekiti. Katika uwanja wa Qatar ambao una matengenezo, je, unaweza ukapanuliwa mpaka ukawa *stand* namba mbili, ukiacha ile moja kwa kipindi hiki mpaka *stand* kubwa itakapopatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema mwanzo kwamba *stand* ile iliyopo Qatar sasa hivi haitoshelezi, lakini sisi kazi yetu ni kuambiwa kwamba kuna sehemu tayari na Baraza la Mji wameshaiona, baada ya kukaa wizara tatu nilizozitaja kabla, sisi kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 2003, sisi kazi yetu ni kuitangaza ile sehemu. Lakini ushauri wake tunauchukua tutaupeleka kunakohusika na tunaufanyia kazi kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu, ili kuonekana kwamba sisi serikali tuko hapa kuondosha kero za wananchi na sio kuwatia katika matatizo. Kwa hivyo, nalichukua na nitalifanyia kazi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kuniona na ukanipa nafasi hii asubuhi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Kwa sababu Mji wa Konde ndio Mji Mkuu wa Wilaya ya Micheweni, na kwamba mji huo sasa hauna *stand* kabisa, magari yanaegeshwa pembeni mwa barabara ambapo inaleta dhiki na kero kubwa kwa wananchi, hata pale msafara wa viongozi wakuu unapopita katika eneo hilo.

Je, wizara inaiona hii kama ni kero, na lini itatatua kero hii kwa kuupatia *stand* Mji wa Konde ili kuondoa usumbufu unaotukabili watu wa Konde.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Ni kweli tunajua tatizo lililopo pale Konde, na kama nilivyosema mwanzo mambo haya yote lazima tukae Wizara tatu kulijadili, lakini namuahidi kwamba katika bajeti ya 2016/2017 basi tutahakikisha kwamba si tatizo la Konde tu bali pia la mjini tunalifanyia ufumbuzi yakinifu na vile vile tunatatua kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu.

Kwa hivyo, namuomba atuachie mpaka bajeti inayokuja tukae pamoja na Idara husika au tuseme Wizara hizo tatu ili kulitatua hili tatizo na ninaamini kabisa kwamba matatizo ya *stand* hata sisi yanatuuma na tunataka kuona kwamba hamna usumbufu wala msongamano wa magari si Konde tu bali Wilaya zote za Zanzibar.

Kwa hivyo nitalifanyia kazi na nina hakika kwamba litatatulika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza kwa kuwa wananchi wengi hutegemea hizi *stand* kubwa ambazo ni *Main Stands* na vituo vidogo vidogo vya usafiri katika kuhakikisha kwamba wanafika safari zao kutoka eneo moja kwenda jengine.

a) Ni utaratibu gani Wizara imejipangia katika kuhakikisha kwamba katika maeneo yote ya Unguja na Pemba tutakuwa tuna *Master Plan* ya miji kuhakikisha kwamba hizi *Stands* zote zinajulikana katika maeneo, ili maeneo haya yanakuwa hayavamiwi na wananchi katika kujenga maduka.

b) Tumeona wananchi sasa katika Mkoa wa Mjini wa Magharibi wameondoa kile kituo cha *stand* pale Darajani na imeeleta tatizo na kero na pia uchafu na mazingira magumu ya usumbufu kwa kina mama, wanafunzi pamoja katika kutembea kusubiri katika eneo la Afisi ya Chama cha Mapinduzi, Skuli ya Kisiwandui pamoja na mbele ya Skuli ya Haile Selassie mpaka *block No* 7 la Michenzani.

Je, Serikali haioni huu usumbufu wanaopata wananchi hasa katika usafiri wanaotoka Pemba na kufika Unguja kubeba mizigo yao ya mikungu ya ndizi pamoja na mabegi na watoto, ambayo husababisha

usumbufu na kusababisha pia jina la Rais wetu wa Zanzibar kusemwa na wananchi na Chama cha Mapinduzi vibaya. Ni kitu gani au mawazo gani Serikali imejipanga katika kuondoa matatizo haya ya wananchi hasa katika usumbufu huu na hili balaa ambalo sasa limekuwa kero kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Kama nilivyosema awali tunakubaliana kwamba kuna matatizo ambayo pia sisi tumeyakuta hasa katika mambo ya vituo vya dala dala, lakini mimi napenda kumuahidi tu kwamba avute subra tuna mipango mizuri, na kama ulivyosema mimi nitawaomba sana Wizara ya Ardhi kupitia mipango miji na vijiji watangaze ule mpango mji na vijiji ambavyo tayari upo, ili wananchi wetu wapate kujua ni hasa sehemu gani ambazo tutajenga hivyo vituo na sehemu gani ambazo inatakiwa wao wafanye maeneo ya kujenga kama vituo vya biashara au vituo vyengine vyoyote.

Kwa hivyo, hawa Mipango Miji ramani yao ipo, mimi nitawaomba tu kupitia Wizara ya Ardhi basi watoe elimu kupitia Televisheni au vipindi vyengine vyovyote ili wananchi wapate kuwa na uelewa kuhusu mipango miji na vijiji.

Kuhusu suala lake la pili kama alivyosema sisi tuko katika mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba hizo kero za wananchi zinaondoka, na kama tulivyosema tokea mwanzo ilipangwa kwamba Mji Mkongwe kuondokana na msongamano kile kituo cha Darajani lazima kiondoke, kwa hivyo ndio maana tukaweka vituo sehemu tofauti, kituo cha Malindi kile tutakiboresha ili wananchi wanaotoka bandarini wasipate tabu. Na vile vile tutahakikisha kwamba katika kituo hicho tunachojenga kikubwa cha usafiri wa mabasi basi tunaweka huduma zote za miundombinu ili kuwaondolea kero wananchi wetu, ahsante sana.

Nam. 182

Ongezeko la Wataalamu wa Kilimo

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:

Kwa kuwa Wataalamu wa Kilimo ni nguzo muhimu na tegemeo kubwa kwa wakulima wetu hasa katika kutilia mkazo kilimo bora (kisasa).

(a) Je, Zanzibar tuna mabibi na mabwana shamba wangapi.

(b) Je, kila bibi na bwana shamba mmoja anahudumia wakulima wangapi.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mabibi na mabwana shamba ili wakulima wetu wapate kwa urahisi utaalamu na mbinu mpya za kilimo cha kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 182 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, mfumo wa elimu kwa wakulima katika ngazi ya Shehia unatekelezwa na Bwana/Bibi shamba ambao wanasimamiwa na Afisa wa Kilimo wa Wilaya.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ina jumla ya wafanyakazi mabwana na mabibi shamba 179 (Unguja 135 na Pemba 44). Lengo la Wizara ni kuwa na Bwana/Bibi shamba mmoja kwa kila Shehia, kutokana na upungufu, hivi sasa Bwana/Bibi shamba mmoja anahudumia zaidi ya wakulima 3,000 kwa vile anahudumia zaidi ya Shehia moja.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina Shehia 384 ukitoa 55 za Mjini Unguja tunabakiwa na Shehia 329 (Unguja 200 na Pemba 129). Takwimu zinatuonesha kuwa tuna upungufu wa mabwana na mabibi shamba 150 (Unguja 85 na Pemba 65) ambao wanahitajika ili kufikia kila Shehia. Hivyo, Serikali itaendelea kusomesha na kuajiri Bwana/Bibi shamba, kama ambavyo imeelezwa katika *Programme SLO* 10101/2 Utafiti na Mafunzo ambapo kwa mwaka huu tutafunza vijana 70. Sambamba na programu nyengine za mafunzo ili tujaze upungufu uliopo wa Bwana/Bibi shamba katika nchi yetu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Nataka nijue tu kuna tofauti gani baina ya Mabwana Shamba na Mabwana Ugani.

b) Katika majibu yako umesema kuna Mabwana Shamba 179 lakini hao Mabwana shamba 179 kwa nini wanaendelea kufanya kazi kwa mazoea kwa kubaki sana maofisini na hawaendi kwa wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti swali lake la kwanza alisema anataka kujua tofauti ya Mabwana Shamba na nani sijamsikia hilo

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mabwana Ugani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mabwana Ugani sielewi jina hilo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nitaanza na kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi nitaanza na swali lake la (b) kama ifutavyo.

Mheshimiwa Yussuf Mabwana Shamba tulionao ni wachache, ningewashauri wakulima wakawa na mazoea kama wafugaji, anapoumwa ng'ombe anapelekwa ng'ombe kwa daktari na kutibiwa, na wao ningewashauri wakawa wanakwenda kwa wale mabwana Shamba wilayani kwa kueleza matatizo yao ili waweze kutusaidia na sisi ule uhafifu tulionao wa Mabwana Shamba na Mabibi Shamba.

Suala lake la (a) tofaufi ya Mabwanashamba na Ugani ningeomba Mhe. Waziri anisaidie.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa *PAC* maana yake ana kazi kubwa sana kwa swali lake la nyongeza.

Ukweli hizi ni *terminologies* tu zinatumika zaidi lakini watu wa ugani ni wale ambao wako kwenye Wilaya na wanashughulika na maeneo makubwa sana, wale bwana shamba ni wale ambao wako katika vituo mbali mbali ndio maana tunakwenda mpaka kituo cha chini, hata taaluma zao ni tofauti; bwana Ugani ana taaluma kubwa zaidi kuliko yule bwana shamba hiyo ndio tofauti kubwa tu iliopo, lakini ni suala la taaluma, huyu mmoja ana taaluma kubwa zaidi mwengine ana taaluma ndogo kidogo.

Niongezee tu kwa kusema kwamba huu upungufu tulionao baada ya uzoefu ambao nimeukuta juzi Tumbatu bwana shamba ambaye yuko pale inaonekana wazi kabisa wananchi hawamtumii vizuri, kwa hivyo wanasubiri wao aende kuwahudumia wewe mwenye shida huendi ukamwambia nina shida fulani, tofauti na wa mifugo, mifugo mtu akiharibikiwa na ng'ombe wake anakwenda

kumtafuta bwana mifugo. Sasa mimi nafikiri umefika wakati sasa kwanza hawa wakulima wetu wachukue bidii ya kuwatafuta hawa wataalamu wapate taaluma zao, wasimngojee tu yeye akakaa ofisini n.k.

Halafu kuna suala ambalo limeulizwa kwamba watu wetu wanakaa sana ofisini hawaendi, ni kweli kabisa tulikuwa na utaratibu watu wetu wengi hawafiki kwenye vijiji, ndio maana sasa tumejipangia tokea Afisi Kuu mpaka chini asilimia 70 kwenye *field* na asilimia 30 Afisini.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuavyo lenye sehemu (a) na (b).

a) Sera ya Kilimo inaeleza pawepo na Mabwanashamba na Mabibishamba mmoja kila wilaya. Shehia ngapi hivi sasa zenye wataalamu hao Unguja na Pemba.

b) Unajua kwamba Mabwana Shamba wengi wanapenda kukaa ofisini na kutokwenda *field* kuwashauri wakulima. Je, Wizara yako inachukua hatua gani kulikabili tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mheshimiwa Shadya swali lako la mwano kwa vile ni la takwimu naomba nitakujibu kwa maandishi la (a).

Na swali la (b) kama alivyosema Mhe. Waziri, asilimia 70 tumeamua kufanya kazi *field*, kwa hivyo sisi kama wakuu wa Wizara tumeamua hivyo basi tutahakikisha Mwabwana Shamba na Mabibi shamba tupate wakamilifu kwanza tutimize kwenye shehia halafu waweze kuwapitia wakulima wetu kama kawaida. Pia kwa kusaidiana kazi hii basi kwa vile tunao wachache wasikae tu na tatizo lakini waende kwenye Wilaya kuonana na hawa Mabwana shamba na Mabibi shamba ambao wapo.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti kuna tatizo la hao mabwana shamba wachache kwamba wanaishi mjini lakini maeneo ya kazi waliyopangiwa yako vijijini. Na ushahidi kuna bwana shamba yuko mjini lakini eneo la kazi liko Kijini na hana usafiri wala hana nyumba ya kuishi kule.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa mabwana shamba wa aina hii kuwapatia vipando au kuwajengea nyumba katika maeneo ambayo wanafanyia kazi, aidha kuwapata mabwana shamba ambao wanaishi katika maeneo yale yale ili kuwasaidia wakulima.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kutokana na ukosefu tulionao hawa Mabwana shamba tutahakikisha ajira tutakazozitengeneza sasa tutawaajiri wale watu husika wa yale maeneo ili kurahisisha kazi zetu ziende kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri naomba kumhakikishia Mhe. Rashid kwanza tumeshafanya *survey* kuhakikisha watu wetu wote ambao hawakai na wakulima kule ambako wamepangiwa kazi, wachague ama wabaki kwa wakulima au wabaki mjini kufanya kazi zao mjini, wachague, atakayebaki kwa wakulima atabaki kwenye ajira, yule ambaye atabaki mjini abaki kufanya shughuli zake za mjini, hilo la kwanza.

La pili wiki ijayo au wiki mbili zijazo tutaanza kutoa piki piki kwa Mabwana shamba wale ambao wameamua kukaa kwenye vijiji, kwa hivyo vifaa vya kufanyia kazi vipo tutawapatia, lakini nasema kabisa Bwana shamba ambaye hawezi kukaa pale ambapo kuna mazingira yake ya kazi tutamsamehe tupate watu ambao wanaweza kufanya kazi kwa kuwatumikia watu.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuna tangazo la wageni katika ukumbi wetu tuna wageni. Tunaye mgeni wa Mhe. Suleiman Makame Ali kutoka Jimbo la Ziwani ambaye anaitwa Ali Khamis Ali kutoka Jimbo lake la Ziwani, ahsante karibu sana.

Waheshimiwa Wajumbe naomba nikumbushe tu baada ya kumaliza suala la hoja itakayoletwa Wajumbe tuwe tayari kwa kurudi kwenye ukumbi wa juu kuendelea na ile semina ambayo imeshatangazwa tokea juzi, mahudhurio ni muhimu sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja 2016

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti naomba kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote kuwepo hapa leo tukiwa na afya njema na wazima kabisa.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kutupatia fursa hii adhimu, naomba nitakapokutamka Spika utanichukulia nakusudia Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa kama Kanuni za Baraza zinavyotutaka, nisome Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza, inasema kama ifutavyo:

"Endapo shahada iliyotiwa saini na Mhe. Rais itawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri akitamka kwamba Mswada wa Serikali ni wa dharura na wa haraka sana, hata kuwa haiwezekani kutimiza masharti ya Kanuni ya 79, basi masharti hayo yatawekwa kando kwa ajili ya mswada huo, hivyo kanuni ya 79 itasita mara moja kutumika bila ya hoja yoyote."

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba tena kusoma Shahada maalum ya kuwasilisha Mswada wa dharura ambayo ipo chini ya kanuni hii ya 80 ambayo imesainiwa na Mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na naomba ninukuu kama ifuatavyo:

" Kwa uwezo aliopewa Mhe. Rais chini ya kanuni ya 80 ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar mwaka 2012. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anatamka kwamba Mswada wa Sheria ya kuanzisha Hospitali ya Mnazi Mmoja na mambo yanayohusiana na hayo ni wa dharura na wa haraka sana kutokana na sababu kuu mbili zifuatazo."

Sababu ya kwanza kufuatia mapendekezo ya Nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ndio Hospitali Kuu kwa hapa Zanzibar inahitajika kuwa na hadhi ya kisheria ili kukidhi vigezo vya kuwa Hospitali Kuu na iwe na uwezo wa kutoa mafunzo ya matibabu.

Pili, kila nchi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki itahitajika kutekeleza mapendekezo hayo ndani ya kipindi cha miezi sita ambapo kwa sasa muda uliobaki kwetu sisi ni mfupi mno kufikia kumalizika kwa muda huo. Hivyo mswada huo haitowezekana kuwasilishwa kujadiliwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa kufuata utaratibu wa kawaida chini ya masharti ya kanuni ya 79 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo kwa kuzingatia sababu hizo naomba kuwasilisha shahada hii ya dharura, ili Baraza la Wawakilishi la Zanzibar liweze kujadili na kuupitisha mswada wa sheria ya kuanzisha hospitali ya Mnazimmoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo kwa sababu zilizotajwa kwa kutumia utaratibu uliowekwa chini ya Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar mwaka 2012. Imetiwa saini na mhuri wa Rais Ikulu Zanzibar tarehe 21 Juni, 2016 Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyaeleza hayo mambo ya kisheria naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Mswada huu wa Sheria ya Kuanzishwa Hospitali ya Mnazimmoja kuwa Taasisi inayojitegemea, hatua ambayo itafanya hospitali hii kutambulika kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, nitaomba kwanza nianze na utangulizi ambao utakuwa na historia fupi juu ya hospitali ya Mnazimmoja. Hospitali ya Mnazimmoja ilianzishwa rasmi mnamo mwaka 1920 yaani 2020 itatimiza miaka 100 hospitali hii ikiwa na jina la Sewa Haji. Hospitali hii ilijengwa ikiwa na madhumuni ya kuwahudumia wananchi wa Zanzibar na ilianza kwa huduma za matibabu katika jengo *cot ward* umaarufu kwa jina la hospitali ya mbao, ambayo hivi sasa ipo katika hali ya kutaka marekebesho. Na huyu ndugu Sewa Haji alikuwa ni mfanya biashara maarufu hapa Zanzibar mwenye asili ya kibohora. Baadaye katika mwaka 1956 jengo kubwa la ghorofa tatu yaani *main building* lilikuwepo sasa lilijengwa na bwana Hasanali Karimjii Jivanjii, ambaye alikuwa ni mfanya biashara maarufu hapa Zanzibar kwa wakati huo na pia naye ni mwenye asili ya kibohora.

Kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964 hospitali hii ilikuwa na jumla ya vitanda 277 vya kulaza wagonjwa mbali mbali, uwezo huo baada ya Mapinduzi uliongezwa na kufikia vitanda 300. Mnamo tarehe 3 Julai, mwaka 1964 Baraza la Mapinduzi lilitoa warka nambari 37 ambao ulikuwa na mambo 17 muhimu. Na haya ninayaeleza Mhe. Mwenyekiti, kwa faida ya wale waliokuwa wakihoji juu ya warka huu. Mambo hayo yalihusu kuimarisha sekta ya afya na miongoni mwa hayo ni kuwepo kwa hospitali kuu moja katika kila kisiwa cha Unguja na Pemba.

Serikali kwa wakati huo iliendelea na jitihada za kuimarisha hospitali ya Mnazimmoja kwa kuiongezea idadi ya vitanda na kusomesha wataalam mbali mbali, akiwemo Dkt. Ali Mohammed Shein mwenyewe wakati huo.

Katika miaka ya 1970 hospitali ilifanyiwa matengenezo makubwa ikiwemo yale ya jengo kubwa la kulaza wagonjwa ambalo wakati huo lilipewa jina la Vladimir Ilyich Lenin au kwa lugha yetu ya kawaida V. I. Lenin.

Mhe. Mwenyekiti, mnamo mwaka 1997 hospitali ya Mnazimmoja chini ya ufadhili wa Serikali ya Abudhabi ilifanyiwa matengenezo mengine makubwa yaliyohusisha majengo pamoja na kuweka vifaa vya kisasa ambapo uwezo wake wa kulaza wagonjwa sasa uliongezeka na kufikia vitanda 400. Katika awamu mbali mbali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendelea kufanyia matengenezo hospitali hiyo na kuipatia vifaa vya kisasa na wataalam mbali mbali ili ifikie kiwango cha hospitali ya rufaa kilichokusudiwa. Dhamira hiyo pia ilikusudia kuimarisha huduma za kinga na tiba pamoja na kuwa na lengo la kuanzisha kitengo cha kushughulikia maradhi yatokanayo na matatizo ya figo.

Maradhi mengine ambayo serikali imekuwa na dhamira ya kushughulikiwa hapo Mnazimmoja ni maradhi ya moyo, saratani, na huduma nyengine mbali mbali za tiba. Hatua kadhaa zinaendelea kuchukuliwa ikiwemo kuipandisha hadhi hospitali hii na kuwa idara kamili mnamo mwaka 2004.

Mhe. Mwenyekiti, dhamira ya kuifanya hospitali ya Mnazimmoja kuwa hospitali ya rufaa na yenye kujitegemea iliendelea na ilielezwa katika sera ya mwanzo ya Wizara ya Afya mnamo mwaka 1990 na kusisitizwa tena mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba mara tu baada ya kuingia madarakani ilisisitiza tena nia ya serikali ya kuendeleza na kuendelea kuipandisha hadhi hospitali hiyo ya Mnazimmoja kama ilivyothibitishwa tarehe 11 Novemba, 2010 kupitia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein wakati wa uzinduzi wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi la Nane na kurudiwa tena katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la Tisa ya tarehe 5 April, 2016 iliyotolewa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada ya kutekeleza azma hiyo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein katika ufunguzi wa jengo jipya la huduma za ubongo na uti wa mgongo yaani *Neurosurgery Unit* lilioko pale Mnazimmoja tarehe 10 Januari, 2015

tukisherehekea miaka 51 ya Mapinduzi aliendelea kusisitiza tena azma ya serikali ya kuifanya hospitali ya Mnazimmoja kuwa yenye kujitegemea na kukumbusha uwasilishwaji wa haraka wa waraka husika serikalini wakati huo, ambao leo huu ndio unawasilishwa hapa Barazani kama mswada.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo ya serikali Wizara ya Afya iliwasilisha nyaraka katika vikao mbali mbali serikalini ikiwemo kamati ya Makatibu Wakuu na hatimaye kuridhiwa na Baraza la Mapinduzi la tarehe 28 Mei, 2016 hatua ambayo imepelekea uwasilishaji wetu huu wa leo.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Mnazimmoja inazo Kliniki maalum kwa hivi sasa kama vile Kliniki ya Koo, Kliniki ya Macho, Kliniki ya Akinamama, Kliniki ya Kisukari, Kliniki ya Shindikizo la Damu na Matibabu mbali mbali kupitia mazoezi ya viungo yaani *Physiotherapy Unit,* Kliniki hizi zina jukumu la kutoa huduma mbali mbali za tiba na ushauri kwa wagonjwa husika.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwaka 2004 hospitali ya Mnazimmoja ilikuwa ikiendeshwa chini ya Idara ya Tiba na baadae ilipewa hadhi ya kuwa Idara kamili mwaka huo huo kwa lengo la kuiongozea ufanisi katika kutoa huduma zake. Tangu kuanzishwa kwake Idara hii ya Mnazimmoja imekuwa ikijumuisha hospitali tatu ambazo ni; Hospitali Kuu yenyewe ya Mnazimmoja, Hospitali ya Wazazi Muembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo chekundu. Hivi sasa Idara ya Hospitali ya Mnazimmoja naomba hapa nikizungumzia Mnazimmoja tafadhali isijulikane kwamba lile eneo lililokuwepo pale Maisara tu, naomba ieleweke Muembeladu na Kidongo chekundu zote katika fungu hilo hilo moja.

Hivi sasa Idara ya Mnazimmoja ina jumla ya vitanda 546 kwa pale ni 400 na 146 uki-*combine* Mwembeladu na Kidongo chekundu na inasimamiwa chini ya vitengo tisa kama ifuatavyo:-

1. Kitengo cha Huduma za Wagonjwa wa Nje, yaani *Out Patient*,
2. Kitengo cha Huduma za Upasuaji, *Surgery*,
3. Kitengo cha Maradhi ya Akinamama yaani *Obstractics and Gynaecology*,
4. Kitengo cha mazoezi ya viungo na Utengenezaji wa Viungo Bandia yaani *Physiotherapy Unit and rehabilitation.*
5. Kitengo cha Maradhi ya Watoto *Pediatric*,
6. Kitengo cha Maradhi ya Ndani *Internal Medicine*,
7. Kitengo cha Vipimo na Uchunguzi, *Diagnostic Serves*, ndio ile umaarufu inaitwa *Labour*

8. Kitengo cha Huduma za Afya ya Akili, *Psychiatric and Mental Health* hivi vinatolewa kule Kidongochekundu.

9. Kitengo cha Matibabu ya Meno na Afya ya Kinywa yaani *Dentistry*.

Hivyo ndio vitengo vya Mnazimmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Afya ya mwaka 1990 ilitamka haja ya kufanya hospitali ya Mnazimmoja iwe ni hospitali yenye kujitegemea ambayo itatumika kutoa huduma za uchunguzi wa maradhi na matibabu kwa wananchi wetu wote.

Pia, hospitali hiyo itakuwa ni kituo cha kufundishia wanafunzi mbali mbali wa kada za afya pamoja na kufanya tafiti zinazohusiana na masuala ya afya. Hospitali ya Mnazimmoja ilikuwa ikiendeshwa kama nilivyoeleza hapo awali chini Idara Tiba hadi mwaka 2004 ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendelea na jitihada zake za kuipandisha hadhi hospitali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Kitivo cha Tiba katika Chuo Kikuu cha Taifa SUZA miaka 3 iliyopita ili kuweza kutatua tatizo kubwa la upungufu wa madaktari wetu wenyewe wa kizalendo uliokuwa unatukabili. Uamuzi huo ulikuwa mzito na tunamshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein aliendelea kuchukua uamuzi huo. Kitivo hicho kinaendelea vizuri pamoja na changamoto kadhaa ambazo kinakabiliana nazo hivi sasa. Hospitali ya Mnazimmoja hutumika kufundishia wanafunzi hao wa udaktari bila ya kuwa na sheria rasmi hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, Mawaziri wa Afya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walipokutana mjini Arusha mwaka jana walijadili namna ya kusimamia ubora wa mafunzo ya udaktari katika Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki ambapo sisi tunahitaji vijana wetu wawe wanatambulika pamoja na shahada zao za udaktari ziwe zinatambulika. Baada ya majadiliano hayo Mawaziri wa Afya wote walikubaliana kuyapa majukumu Baraza linalosimamia taaluma ya udaktari ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kufanya tathmini ya vyuo vinavyofundisha udaktari katika kanda hii pamoja na hospitali zitakazotumika kufundishia madaktari hao kama zinakidhi viwango au hazikidhi viwango vilivyowekwa kikanda na kitaifa. Mojawapo ikiwa Chuo Kikuu chetu cha SUZA na hospitali ambayo inatoa mafunzo ya Mnazimmoja kwa hapa Zanzibar.

Mabaraza hayo yanayodhibiti taaluma ya udaktari ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yalikutana mwezi wa Julai, mwaka 2015. Zanzibar ilishirikishwa moja kwa moja kama nchi kuangalia namna ya kudhibiti na

kuimarisha taaluma ya udaktari kwa kuweka vigezo ambavyo vinafanana kwa nchi zote za Jumuiya hiyo kama ambavyo ilivyopendekezwa na Baraza la Mawaziri wa Afya wa Jumuiya hiyo ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, timu za ukaguzi ziliundwa na wajumbe 3 kutoka kila bodi ya nchi wanachama walishiriki na naomba niseme kwa bahati nzuri mjumbe mmoja alitokea Zanzibar moja kwa moja ni Dkt. Jamala Adam Taib, ni fahari kubwa sana kwetu sisi Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupata mjumbe moja kwa moja kwenye *The Highest Council of Education in Medicine* kama *inspector*. Katika mkutano huo ulikubaliwa kutengeneza vigezo ambavyo vitumike kuvikagua vyuo vyote vikuu vitakavyotoa taaluma ya udaktari ambavyo vimepewa usajili na kuendesha mafunzo hayo na mamlaka za nchi husika, pamoja na hospitali ambazo hufundishiwa hawa madaktari katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Hapa nitaomba kidogo nitoe maelezo ya ziada kwa zile *courses* zinazotolewa za *medicine*, lazima *practical* yake yote ifanyike hospitali hamna *laboratory* yaani *laboratory* ya hospitali *physical live practical* inatakiwa ifanyike hospitali. Ndio maana utakuta kila *course* ya udaktari lazima iwe na hospitali ambayo inaitwa *University Hospital* ama *Teaching Hospital* inayosaidia *course* ile ya afya moja kwa moja. Kwa hivyo *course* inatolewa SUZA *State University of Zanzibar* ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu, lakini *practical* zao zote zinafanyika kupitia hospitali ya Kuu ya Mnazi mmoja.

Kazi ya kukagua vyuo hivyo pamoja na hospitali ilipewa Bodi zinazosimamia taaluma ya udaktari, Jumuiya ambazo zinashirikisha nchi 5. Ukaguzi ulifanyika katika nchi zote na Tanzania ilikaguliwa mwezi wa April, mwaka huu 2016. Katika ukaguzi huo baadhi ya mapungufu yalibainika lakini kubwa kabisa ilikuwa ni hospitali ya Mnazimmoja kukosa sheria rasmi yenye mashiko inayoipa mamlaka ya kuwa na hadhi kama hospitali kuu inayotumiwa kufundishia madaktari.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hiyo iliwasilishwa kwa wakuu wote wa vyuo pamoja na wakuu wa nchi husika kwa ajili ya kuzifanyia kazi. Kutokana na taarifa ya ukaguzi huo Serikali ilipewa muda wa miezi 3 ili iweze kurekebisha kasoro hizo ambazo kama hazijarekebishwa zitaweza kuathiri mwenendo mzima wa mafunzo wa madaktari wetu ambayo yameanza kutolewa katika visiwa vyetu vya Zanzibar hivi sasa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeshaunda kikosi kazi kwa ajili ya kuzifanyia kazi kasoro zote zilizoainishwa katika ukaguzi huo. Naomba niseme

humu Barazani katika kikosi kazi hicho yumo Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, yumo Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, yumo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, yumo pia Mhe. Waziri wa Afya. Hatua mbali mbali za utekelezaji zimeshaanza kuchukuliwa. Naomba niongezee hapo pamoja na Makatibu wa Wizara zote hizo Makatibu Wakuu na baadhi ya hatua hizo ni mswada huu ambao nauwasilisha leo hii mbele yako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo yote juu ya mswada huu wa sheria, nawaomba kwa heshima na taadhima na unyenyekevu mkubwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi kuujadili mswada huu, kuuchangia ipasavyo na kuukubali mwisho wa siku ili tuupitishe na serikali iweze kuendelea na hatua zake za utekelezaji kwa ajili ya faida ya wananchi wetu wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu sote tunatumia Chuo Kikuu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Baada ya kuwasilishwa Mswada wa Sheria ya kuanzishwa hospitali ya Mnazimmoja ninafikiri ni shughuli yetu ya leo kutokana na ratiba ya kikao. Sasa suala la kuwasilisha Hotuba ya Kamati ninafikiri haimo katika ratiba.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini maelezo ya jambo hili limeshatolewa jana kwamba leo linawasilishwa tu ili tupate muda wa kwenda kuusoma huu mswada. Sasa Mwenyekiti nae ana nafasi ya kuweza kuja kuleta maoni yao.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa Mheshimiwa, kwa nini ya Waziri imetiwa humu ya Kamati isitiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kwa mujibu wa Kanuni inaruhusu hata kama kwenye *order paper* haimo lakini kiti kinaruhusu kuweza kumruhusu Mwenyekiti na yeye alete maoni yake. Mwenyekiti karibu.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana na kujadili mswada huu muhimu wa kuanzisha Hospitali ya Taifa ya Mnazi Mmoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitangulie kusema kuwa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake ya Baraza la Wawakilishi inaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuleta mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kusimamia na kutekeleza mfumo mzima wa utoaji wa huduma ya afya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika sekta ya afya nchini inakabiliwa na changamoto nyingi katika utendaji wake, sasa kwa namna moja ama nyengine sheria hii itakapoanza kutumika itasaidia kuzitatua baadhi ya changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila endapo sitowashukuru wadau ambao kamati yetu ilikutana nao kuujadili mswada huu kwa undani na kutupatia maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisadia kamati kutoa mapendekezo muhimu katika marekebisho tuliyoyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya huduma za afya, ni wazi kuwa kuna haja kubwa ya kuanzisha sheria hii ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kutoa huduma bora zaidi katika hospitali yetu kuu ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, hospitali inayoanzishwa itatoa huduma kama rufaa na kuweka mfumo mzuri wa utoaji huduma ya afya hapa Zanzibar na itakua na jukumu la kusimamia uendeshaji wa hospitali nyengine yoyote itakayokuwa chini ya usimamizi wa hospitali hii kwa mujibu wa sheria hii au sheria nyengine yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kuimarika kwa sekta ya afya kutaongeza imani ya wananchi kwa serikali yao ambayo inafanya kazi kubwa ya kusimamia misingi ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yaliweka wazi umuhimu wa wananchi kupatiwa huduma bora za matibabu ambazo zitatolewa kwa kila mwananchi bila ya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la kuifanya hospitali hii ni kuwa Hospitali ya Taifa ya Rufaa inayojitegemea chini ya Wizara ya Afya (*Semi - Autonomous*). Hospitali hii ya Taifa ya Rufaa itaendelea kutoa huduma za afya kwa wagonjwa bila ya malipo kwa kufuata sera na miongozo ya wizara. Vile vile, Hospitali hii ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kwa kufikia lengo la kujiendesha na kutoa huduma zilizo bora zaidi itaandaa utaratibu wa kuchangia kwa baadhi ya huduma za afya zinazotolewa na hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii iliupitia mswada huu kwa umakini na kufanya marekebisho kadhaa katika baadhi ya vipengele. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mapendekezo ya kamati kuhusiana na mswada huu, naomba kwanza nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
4. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
5. Mhe. Massoud Abrahman Massoud - Mjumbe
6. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
8. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
9. Ndg. Aziza Waziri Kheir - Katibu
10. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ya kamati yaliyofanywa na kamati yetu. Aidha, naomba niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kuwa, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na kamati. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo naomba muangalie katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 1 cha mswada huu kinachohusiana na jina fupi na kuanza kutumika, kamati imependekeza jina la sheria hii liwe ni Hospitali ya Taifa ya Mnazi mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 2 cha mswada kinachohusiana na ufafanuzi, kamati inapendekeza neno “Hospitali ya Mnazi Mmoja” litolewe ufafanuzi ili ijulikane dhahiri kuwa endapo itasemwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Mnazi Mmoja peke yake au na idara zake kama ilivyo sasa. Aidha, kamati imeomba maneno “rufaa” na “wakala” pia yatolewe ufafanuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia inapendekeza katika Sehemu ya Pili ya Mswada huu ambayo inahusiana na kuanzishwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na kazi zake, kamati imetoa mapendekezo katika kifungu cha 4 kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 4(c) neno “ya kidaktari” yaliyopo mwishoni mwa kifungu hiki yafutwe na badala yake yawekwe maneno “kinga na tiba”. Sababu ya kutoa mapendekezo hayo ni kuwajumuisha watu wote wanaohusika na utoaji wa huduma za afya na isije ikaonekana kuwa walioguswa na sheria hii ni madaktari pekee.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 4 (n) kamati yetu inapendekeza neno “kuibuka” lifutwe na badala yake liwekwe neno “kinga”. Sababu ya pendekezo hili ni ukweli kwamba sio kazi ya hospitali kusimamia na kudhibiti kuibuka kwa maradhi ya mripuko isipokuwa hospitali inaweza kushajihisha wananchi kujikinga na maradhi mbali mbali ya miripuko.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu ya Mswada huu katika kifungu cha 5 (e) Kamati ilipendekeza mwishoni mwa kifungu hicho yaongezwe maneno “kwa kuzingatia jinsia” ili kutoa nafasi sawa baina ya wanawake na wanaume.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 14 maneno ya pembeni ya kifungu hicho yanahamishwa na kupelekwa katika kifungu cha 15, na maneno ya pembeni ya kifungu cha 15 yanahamishiwa katika kifungu cha 14. Hivyo, maneno ya pembeni ya kifungu cha 14 yanasomeka “Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji” na kifungu cha 15 yanasomeka “Sifa za Mkurugenzi Mtendaji”.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 15 (b) kamati imependekeza kuongezwa kwa maneno “kutoka kwenye chuo kinachotambulika” mwishoni mwa kifungu hiki ili kuepusha udanganyifu ambao unaweza kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa tunaiomba serikali kuyazingatia yale yote yaliyopendekezwa na kamati baada ya kupata ushauri mzuri wa wadau wa taasisi mbali mbali ambao kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa maoni yao ili kuifanya sheria hii itakapoanza kutumika iwe bora zaidi. Kufanya hivyo ni kuisaidia serikali na taasisi husika kuepukana na adha na usumbufu uliokuwa unajitokeza kwa wananchi wakati wa upokeaji wa huduma ya afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inapenda kuishauri wizara kukipa meno chombo hiki kipya, kuweza kuajiri na kutoa adabu kwa wasiofanya kazi inavyostahiki (*hire & fire*). Pia kamati inaishauri serikali kushirikiana na sekta binafsi kupitia taasisi mbali mbali za afya ili kuimarisha sekta hii na hatimae kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wauchangie, waukosowe na waurekebishe mswada huu kwa kutoa

mawazo yatakayosaidia katika kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha ili usaidie kuleta ufanisi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru Mhe. Waziri kwa kusoma mswada huu muhimu sana katika nchi yetu kwa afya zetu na watu wetu. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akisoma alisema yeye ataeleza kwa kifupi, lakini tuangalie kwenye marekebisho. Kwa bahati mbaya, marekebisho hayajakuwa *circulated* humu ndani ya Baraza, hii inaweza ikaja ikatuletea *impact* nyengine vile vile. Sasa nilikuwa naomba hasa kutokana na muda wenyewe mdogo, kwa kuwa tutabakia kwenye semina kama hayo marekebisho yapo basi yazalishwe ili tuweze kupatiwa, ili tunapopendekeza mapendekezo yetu tuangalie na marekebisho ya kamati. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamza, hili limeshaonekana na linafanyiwa kazi, kwa vile bado tupo utapatikana kwa wakati *in shaa Allah*.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwatambue wageni wetu wengine wa leo tarehe 28/06/2016, wageni wa Mhe. Haroun Ali Suleiman kutoka Ras Al-Khaima jumla yao ni saba (7). Naomba niwatambue:

1. Mr. Kamal Ataya
2. Mr. Joseph Haskel
3. Mr. Ossama Abdel-Aah
4. Mrs. Sofia Sattarova
5. Mr. Damascene Makatu
6. Mr. Anayaty Tahir
7. Mr. Amani Mworia

Ahsanteni wageni hawa wote wakiongoza na Mr. Ali Khalil Mirza - Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira. Ahsante sana na karibuni sana.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna tangazo jengine hapa; Mhe. Maudline Cyrus Castico - Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ametoa nakala za vitabu vya taarifa ya utekelezaji wa haki na ustawi wa mtoto kwa mwaka 2015/2016, na nakala ya taarifa kuhusu tamko la maadhimisho ya siku ya ushirika duniani katika Baraza la Wawakilishi. Kutokana na kuchelewa

kuchapishwa kwa vitabu hivyo na kwa mujibu wa ratiba ya shughuli za mkutano huu, muda uliobaki kumalizika shughuli zetu ni mdogo sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hakuweza kuwasilisha mbele ya Baraza hili taarifa hizo, hivyo Waheshimiwa Wajumbe mnaombwa sana kuzipitia taarifa hizo, ili mupate uelewa wa kutosha kuhusu masuala yaliyomo ndani yake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa majukumu yetu katika kamati zetu za Baraza kwa ujumla. Ahsanteni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo tumemaliza sasa hivi na muda bado tunao lakini hatuna kingine chochote cha kuendelea nacho, naomba tuweke kanuni kando ili tuendelee na shughuli nyengine tulizopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji, wale ambao wamekubali kutengua kanuni wanyanyue mikono, wasiokubali, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 4:56 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 29/06/2016 saa 3:00 asubuhi)